# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL

# REVISION MOCK EXAMS 2016

## TOP NATIONAL SCHOOLS

**NAIROBI SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## NAIROBI SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**
**Karatasi ya 1**
**Mwongozo wa kusahihisha**

Hii ni ripoti. Vipengele viwili vikuu vya utungo huu ni maudhui na muundo (sura)

a) Muundo (sura)
   Vipengele vifuatavyo vya kimuundo vijitokeze
   i) Kichwa- kionyeshe kamati, ripoti yahusu nini, mahali na kipindi cha kushughulika utafiti huu
   ii) Utangulizi- ulenge yaliyotukia nakusasababisha hata ya uchunguzi, wanajopo husika, mbinu za kukusanya data.
   iii) Mwili- sehemu hii iwe na vijichwa vinavyobeba maudgui
   iv) Hitimisho- hurejelea matokeo ya uchunguzi, yaani muhstari way ale yalioelezwa. Changamoto
   v) Mapendekezo- maoni ya uelekezi wa wanajopo katika utatuzi wa kiini cha tatizo lao.
   vi) Kujitambulisha
      – jina la katibusahihi
      – sahihi
      – tarehe ya uandishi wa ripoti
      –

b) <u>Maudhui</u>
- Kiwango cha usafi na afya ya wapishi kisichoridhisha
- Maji machafu ya mabomba yasiyotibiwa
- Uhifadhi na utunzaji wa chakula maghalani usiofika kiwango kinachokubalika cha usafi
- Takataka kurundikiwa karibu na mazingira ya sehemu za jikoni
- Chakula kilichotayarishwa kwa njia duni
- Uporo
- Kupikiwa chakula chenye sumu ya mgando
- Viungo vilivyopita kiasi
- Kuwepo na viini viletavyo magonjwwa ya kuambukiza

<u>Tanbihi</u>
i) Katika kuandika/ kuwakilisha ujumbe, mtahiniwa azingatie wakati uliopita, nafasi ya tatu, umoja au wingi na lugha rasmi. Mtahiniwa sharti aandike kwa njia nya taarifa
ii) Mtahiniwa atoe hoja tano au zaidi ili kukamilisha na kutosheleza maudhui

**<u>Swali ya pili</u>**
Hii ni insha ya methali
Mtahiniwa abuni kisa kinachodhihirisha maana kuwa:
i) Ashirikiaye jambo zuri mapema zaidi yaw engine hufaidika zaidi kuliko waliochelewa.
ii) Himizo mtu asikawie kufanya jambo aliloazimia kulifanya kwani akikawia huenda likawafaidi wengine.
iii) Aanzaye jambo kabla yaw engine ana uewzo mkubwa kufaulu kuliko wajiungao baadaye
iv) Tabia ya uchelewevu huweza kumfanya mtu kuyakosa mambo mazuri
v) Mtu anapopata nafasi ya kujinufaisha hana budi kuitumia

**<u>Tanbihi</u>**
- mtahiniwa katika kisa chake alenge sehemu mbili za methali (i) kutangulia na (ii) manufaa ya kutangulia huko. Akiegemea upande mmoja, asituzwe zaidi ya alama kumi

- mtahiniwa atunae kisa kimoja

**Swali la tatu**

Matokeo mema, mbali na mwalimu mkuu hutegemea;

- Nidhamu ba bidii ya wanafunzi
- Walimu waliohitimu na kuwajibika
- Vifaa vya kutosha shuleni
- Miundo msingi
- Wizara ya elimu kuendeleza ukaguzi na viwango bora vya elimu
- Washauri ndani na nje ya shule
- Mchango wa wazazi
- Wafanyikazi wa shule kutoa huduma bora
- Uhusiano mwema na majirani wa shule
- Wadhamini wa shule

**Tanbihi**

- Mjadala huu unaegemea upande mmoja wa kupinga. Mbali na mwalimu mkuu, kuna washika dau wengine ambao mchango wao huchangia pakubwa katika kutengeneza matokeo
- Mtahiniwa atoe hoja tano au zaidi ili kukamilisha na kutosheleza maudhui

**Swali la nne**

- Hii ni insha ya mdokezo inayohitaji mtahiniwa kuyasanisi mawazo yake na kubuni hadithi inayoafikiana na kifungu cha kumaliza kisa. Kisa kionyeshe kuwa mhusika aliweza kufaulu kutokana na usaidizi au mchango wa watu wengine katika maisha yake.

- Usaidizi huu uonyeshe ulimwezesha mhusika huyo kupata utajiri, madaraka au matarjio Fulani ya kimaisha

**Tanbihi**

- Mtahiniwa asipoandika fungu la maneno la kumaliziwa ichukuliwe kuwa ameathirika kimtindo.